# HALMASHAURI YA WILAYA YA KAKONKO

## MPANGO NA BAJETI - HALMASHAURI YA WILAYA YA KAKONKO KWA MWAKA WA FEDHA 2016/17

### 0.0. UTANGULIZI:

Kwa Mujibu wa Sheria ya Fedha Na. 9 ya mwaka 1982 ya Serikali za Mitaa Kifungu cha 53 [1], kinaitaka Mamlaka ya Serikali za Mitaa kuandaa Mpango na makisio ya Bajeti na kupitishwa na Mkutano Mkuu Maalum wa Baraza la Madiwani sio chini ya miezi miwili kabla ya kuanza kutumika kwa bajeti hiyo. Katika mchakato huo Kamati za kudumu za Halmashauri zinawajibika kupitia mapendekezo hayo kabla ya kuwasilisha katika Mkutano wa Baraza la Madiwani.

Kulingana na Mwongozo wa ratiba ya mzunguko wa uandaaji wa mpango na bajeti ya Serikali (New budget cycle) ambayo imeanza kutumika tangu mwaka wa 2013/14 Wizara, Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa (LGAs) zinatakiwa kuandaa na kuwasilisha mapendekezo ya mpango na bajeti zao Hazina kati ya tarehe 08 – 28 Januari ya kila mwaka,.katika kuzingatia maelezekezo hayo ninawasilisha mapendekezo ya Mpango na bajeti kwa Halmashauri ya Kakonko ili yaunganishwe na mengine kupata ya Mkoa kwa mwaka 2016/2017.

Mpango na bajeti kwa mwaka 2016/17 umeandaliwa kwa kuzingatia vipaumbele na mikakati ya kiutekelezaji kama ifuatayo:-

**1.** ***Kuboresha utoaji wa elimu bora ili kuongeza kiwango cha ufaulu na kuwaandaa watoto kuweza kukabiliana na maisha baada ya kumaliza masomo.***

*Dondoo ya mambo ya kiutekelezaji.*

- Ujenzi wa nyumba za walimu za kutosha ili kuwapunguzia walimu adha ya kupanga mitaani katika shule za msingi na sekondari.
- Kukamilisha ujenzi wa maabara ya sayansi katika shule za sekondari kwa kuvipatia vifaa muhimu vya kufundishia na kujifunzia ili maabara hizo ziweze kutumika kwa ufanisi.
- Ujenzi wa madarasa ya kutosha ili wanafunzi wakae darasani kwa idadi inayotakiwa.
- Kuajiri walimu wa kutosha na hasa walimu wa sayansi katika shule za sekondari.

**2.** ***Ujenzi wa Makao Makuu ya Halmashauri ya Wilaya ya Kakonko mjini Kakonko***.

*Dondoo ya mambo ya kiutekelezaji.*

- Kuendeleza ujenzi wa ofisi za Halmashauri ya Wilaya ya Kakonko iwapo fedha za awamu ya pili zitatolewa.
- Ujenzi wa nyumba za watumishi kwa kushirikiana na Shirika la Nyumba la Taifa (NHC) ambalo tumeingia makubaliano nao katika kujenga nyumba 50 mjini Kakonko ambapo 20 ni za Halmashauri na 30 zitakopeshwa kwa watumishi kwa masharti nafuu.
- Upatikanaji wa maji ya uhakika kwa ajili ya mji wa Kakonko
- Upatikanaji wa huduma za Simu na umeme kwa kushirikiana na sekta za Umma na binafsi.
- Upimaji wa viwanja vya kujenga ili kuwezesha wakazi wa Kakonko kuweza kujijengea nyumba bora na kuweka mandhari ya mji katika sura nzuri. Halmashauri italipa fidia ili kutwaa ardhi kwa ajili ya kupima na kuuza.
- Ujenzi wa machinjio, kituo cha mabasi na dampo la kutupia takataka

**3.** ***Kukuza uchumi wa mwananchi na kupunguza umaskini wa kipato ili hatimaye pato la mwananchi (Per capita income) liweze kupanda.***

*Dondoo ya mambo ya kiutekelezaji.*

- Kupima viwanja vya ujenzi wa nyumba bora katika maeneo ya mji wa Kakonko ili wananchi waweze kumiliki viwanja kwa ujenzi wa nyumba bora na kuweza kukopesheka katika taasisi za Fedha.
- Kuboresha biashara za mipakani kwa kuwezesha masoko yaliyopo maeneo ya mipakani kuweza kufanya kazi kwa ufanisi.

**4.** ***Kuboresha kilimo na ufugaji ili kuweza kuwa na tija kwa wakulima. Kilimo ndiyo kazi inayotegemewa na watu wengi katika kuendesha maisha yao. Kuboreka kwa kilimo kunakuwa na mahusiano na maisha ya wananchi.***

*Dondoo ya mambo ya kiutekelezaji.*

- Kuendelea kuboresha skimu za umwagiliaji kwa kuboresha miundombinu ya umwagiliaji na menejementi ya uzalishaji katika skimu hizo ili ziweze kuzalisha kwa tija kubwa zaidi.
- Kuongeza matumizi ya teknolojia bora katika kilimo kwa lengo la kuongeza tija katika uzalishaji.
- Kuendeleza kilimo cha zao la Mnyororo wa thamani (Mpunga) na mazao mengine makuu kama mihogo, mahindi na mazao mapya yanayoonyesha kukubalika na wengi kama alizeti.

**5.** ***Kuboresha ukusanyaji wa mapato ya Ndani ya Halmashauri ya Wilaya ili iweze kujitegemea katika kujiendesha.***

*Dondoo ya mambo ya kiutekelezaji*

- Kuboresha mbinu za ukusanyaji wa mapato ya ndani.
- Kubuni vyanzo vipya.

**6.0 *Kuboresha LISHE kwa wananchi wa Halmashauri ya kakonko***

*Dondoo za mambo ya kiutekelezaji*

- Kupunguza utapiamlo na udumavu kwa wananchi wa Wilaya ya kakonko
- kuzalisha mazao yenye Viamini A kwa wingi
- Kuwahudumia wakina mama wajawazito vizuri ili waweze kujifungua watoto wenye Afya

## 2.0. MAPITIO YA MPANGO NA BAJETI YA MWAKA 2015/16

Halmsahuri ya Wilaya ya Kakonko katika mwaka wa Fedha 2015/2016 ilidhinishiwa kukusanya na kutumia ***Tsh. 16,746,829,070/=*** kwa ajili ya matumizi ya kawaida, mishahara na miradi ya maendeleo. Kati ya Fedha hizo, matumizi ya kawaida ni ***Tsh 1,072,087,000/***=, Mishahara ni ***Tsh 11,955,904,000/=*** na Miradi ya Maendeleo ni ***Tsh 3,278,088,070/=.*** Wachangiaji wa bajeti hii ni Serikali kuu iliyoombwa kuchangia ***Tsh.16,306,079,070/=*** na Halmashauri ya Wilaya ya Kakonko ni ***Tsh. 440,750,000/=***

Hadi kufikia tarehe 31.12.2015 Halmashauri ilikuwa imetekeleza **11%** ya bajeti yake ya mwaka ikiwa ni pamoja na Fedha zilizopokelewa nje ya bajeti kwa mwaka 2015/2016.

**Muhtasari wa Utekelezaji wa Mpango na bajeti kwa mwaka 2015/16**

| **NA.** | **AINA YA MATUMIZI** | **BAJETI** | **UTEKELEZAJI HADI DESEMBA 2015** | **%** |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Ruzuku ya matumizi ya kawaida (**OC**) | 1,072,087,000 | 116,549,000 | 10.87 |
| 2 | Ruzuku ya mishahara (**PE**) | 11,955,904,000 | 1,697,057,116.99 | 14.19 |
| 3 | Miradi ya maendeleo (**Dev**) | 3,278,088,070 | 235,418,290 | 6.03 |
| 4 | Mapato ya ndani (**Own source**) | 440,750,000 | 57,155,565.56 | 12.96 |
| | **Jumla** | **16,746,829,070** | **2,106,179,972.55 (11%)** | |

## 3.0. UTEKELEZAJI WA MPANGO NA BAJETI MWAKA 2016/17

Katika mwaka wa fedha wa 2016/17, Halmashauri ya Wilaya ya Kakonko imepanga kukusanya na kutumia jumla ya ***Tsh. 54,532,878,244/=*** toka vyanzo mbalimbali ikiwemo ruzuku ya Serikali Kuu, ***Tsh. 54,008,704,844/=*** na mapato ya ndani ni Tsh. ***Tsh. 524,173,400/=.*** Aidha mchango wa Serikali ni sawa na **99%** ya bajeti yote ya Halmashauri na iliyobaki 1**.0%** ni Mchango wa Halmashauri.

### 3.1. MAENEO YASIYO YA RUZUKU [VYANZO VYA NDANI] KWA MWAKA WA FEDHA 2016/2017:

Katika mwaka wa fedha 2016/2017, Halmashauri inakisia kukusanya ***TSh. 524,173,400 /=*** kutoka katika vyanzo vyake vya ndani [own source]. Kati ya fedha hizo, Halmashauri inakisia kukusanya ***TSh. 40,000,000*** kutokana na Mfuko wa Afya ya Jamii [CHF], ***TSh. 20,000,000/=*** kutokana na Bima ya Afya (NHIF), ***Tsh. 10,000,000/=*** ada kwa mtumiaji (User Fee). Kutokana na mchanganuo huu, fedha zitakazoingia moja kwa moja katika hazina ya Halmashauri ni ***Tsh. 454,173,400/=***i.

Maeneo makuu yanayotegemewa zaidi na Halmashauri kupata mapato yake ni ushuru wa mazao (***Tsh. 216,722,500/=),*** Ada ya upimaji ardhi (***Tsh. 50,186,400/=),*** ada za leseni za biashara (***Tsh. 23,727,500/=)***, minada na mifugo ***(Tsh 30,790,000/=)*** na Ushuru wa soko (***Tsh. 35,618,000/=).***

### 3.2. MATUMIZI MAENEO YA RUZUKU

#### 3.2.1. MATUMIZI YA KAWAIDA (OC)

Halmashauri inakisia kutumia ***TSh. 3,789,326,662/=*** kwa mwaka wa fedha 2016/2017. Fedha hizo zinajumuisha ***Tsh. 403,670,000/=*** za fidia za kodi ya vyanzo vilivyofutwa ambazo zimeelekezwa zaidi katika eneo la utawala. Halmashauri inaendelea kuomba ununuzi wa magari ambapo kwa mwaka 2016/2017 tumeomba ***1,571,000,000/=***

#### 3.2.2 MISHAHARA (PE)

Katika mwaka wa fedha 2016/2017 Halmashauri imekisia kupokea Ruzuku ya Mishahara ya ***TSh. 12,568,210,424/=.*** Hadi sasa Halmashauri ina jumla ya watumishi **1,020** wakati Ikama inaonyesha kuwa tunahitaji watumishi **1,594**. Halmashauri inatarajia kuajiri watumishi **471** ili kukabiliana na upungufu uliopo na kujaza mapengo yatakayoachwa wazi na watumishi watakaostaafu ikiwa ni kwa mujibu wa sheria No 17.

#### 3.2.3 MIRADI YA MAENDELEO

Kwa mwaka wa fedha 2016/2017 Halmashauri imekisia kupokea kutoka Serikali Kuu kwa ajili ya miradi ya Maendeleo jumla ya ***TSh. 37,651,167,758/=.***

Fedha nyingi zimeelekezwa katika kukamilisha miradi viporo kwani Miradi mipya itakayotekelezwa ni ujenzi wa Makao Mkuu ya Halmashauri, miradi wa maji iliopo chini ya Programu ya Usambazaji Maji vijiji na Usafi wa mazingira, Miradi ya soko , Stendi, dampo madarasa na shule mpya, pia kuendeleza miradi ya skimu ya umwagiliaji na uwekezaji katika sekta ya kilimo.

**Muhtasari wa Utekelezaji wa Mpango na bajeti kwa mwaka 2016/17**

| NA | AINA YA MATUMIZI | BAJETI | % |
|---|---|---|---|
| 1 | Ruzuku ya matumizi ya kawaida (OC) | 3,789,326,662 | 7.1 |
| 2 | Ruzuku ya mishahara (PE) | 12,568,210,424 | 24.1 |
| 3 | Miradi ya maendeleo (Dev) | 37,651,167,758 | 67.8 |
| 4 | Mapato ya ndani | 524,173,400 | 1.0 |
| | **Jumla** | **54,532,878,244/=** | **100.00** |

Maeneo makuu yaliyopewa kipaumbele ni kama ifuatayo:-

1. Ujenzi wa Makao Makuu ya Halmashauri ya Wilaya ya Kakonko na Ujenzi wa Nyumba za Watumishi
2. Ujenzi wa kituo cha Mabasi
3. Ujenzi wa Hospitali ya Wilaya
4. Kuendeleza Programu ya kusambaza maji vijijini na usafi wa Mazingaira kwa kuongeza vijiji 10
5. Kujenga zahanati tano (05), vituo vya Afya viwili (02) na Nyumba za watumishi wa idara ya Afya ili kuweza kutoa huduma bora Zaidi kwa wananchi
6. Kuboresha sekta ya elimu kwa kukamilisha vyumba vya maabara za sayansi katika shule za sekondari, nyumba za walimu na madarasa. Pia kujenga nyumba mpya na madarasa mapya ili kukidhi mahitaji katika kutoa Elimu bora katika Halmashauri
7. Kujenga Dampo ili kuimalisha hali ya usafi wa Mji wa Kakonko
8. Kujenga Machinjio
9. Kuboresha skimu 3 za umwagiliaji, kwa Ruhwiti ili iweze kuwa na tija katika uzalishaji na kwa muhwazi (Bugunga A) na Bugunga B kujenga mabwawa ,mifereji mikuu, vigawa maji na kukarabati barabara za kuingilia kwenye Skimu.

Mchanganuo wa Mpango na Bajeti umefafanuliwa kama ifuatayo:-

1. Umbile la bajeti ukurasa wa 6 hadi 7,
2. Mapato ya vyanzo vya ndani ukurasa wa 8 hadi 15,
3. Matumizi ya kawaida kwa maeneo yasiyo ya ruzuku ukurasa wa 16 hadi 18,
4. Matumizi ya kawaida maeneo ya ruzuku ukurasa wa 19 hadi 30,
5. Mishahara ukurasa wa 31, na
6. Miradi ya maendeleo ukurasa wa 33 hadi 48.

Jaina S Msangi
MKURUGENZI MTENDAJI(W)
**KAKONKO**

MKURUGENZI MTENDAJI(W)
HALMASHAURI YA WILAYA
KAKONKO